# Hongera Mhe. Rais

Tanzania



## CHIFU HANGAYA



**Bw. Nehemiah Mchechu**
Msajili wa Hazina



**Dkt. Venance Mwasse**
Mkurugenzi Mtendaji



**Mha. Hassan Seif Saidy**
Mkurugenzi Mkuu



**Bw. Dennis Simba**
Mkurugenzi Mkuu



**Bi. Asha Dachi**
Mkurugenzi Mtendaji

## Wasifu wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan

Rais wa Jamhuri
ya Muungano
wa Tanzania



# Chifu Hangaya, kinara wa kasi ya maendeleo

*- Na Anna Mwikola -*

**Novemba 3, 2025, Samia Suluhu Hassan ameandika historia nyingine ya kuwa Rais wa kwanza mwanamke Tanzania kuchaguliwa kwa kura za wananchi.**

Chifu Hangaya ni jina alilopewa Rais Samia na jamii ya Wasukuma mkoani Mwanza miezi michache baada ya kuingia madarakani mwaka 2021. Asili ya jina hili ikiwa ni heshima na utambulisho wa uongozi wa kijadi.

Katika utamaduni wa Kisukuma, neno Chifu humaanisha kiongozi wa heshima, mwenye busara na anayelinda maslahi ya watu wake. Neno Hangaya linamaanisha 'anayekusanya na kuleta pamoja', likiwa na tafsiri ya mtu mwenye uwezo wa kuunganisha jamii katika amani na maendeleo.

Kwa kumpa jina hilo, Wasukuma walitambua sifa za uongozi wa Rais Samia hasa uwezo wake wa kuleta umoja wa kitaifa, usawa wa kijinsia na mageuzi ya kiuchumi yenye kujali watu.

Kwa mantiki hiyo, Chifu Hangaya si jina la heshima tu, bali pia ni alama ya uhalali wa kijamii na kiutamaduni inayompa nguvu Rais Samia kuendelea kuongoza Tanzania kwa umoja, amani na maendeleo endelevu.

Wakati wa hafla ya kumuapisha jijini Dodoma Novemba 3, 2025, mizinga 21 inapigwa mara mbili kwa nyakati tofauti. Kwanza inapigwa mizinga ya kuashiria kuachia madaraka baada ya kumalizika kipindi cha kwanza cha utawala wake na ya pili inaashiria kuanza kwa kipindi cha pili cha Awamu ya Sita ya uongozi wa nchi.

Rais Samia alishika madaraka ya urais kwa mara ya kwanza Machi 19, 2021 alipoapishwa akiwa amepokea nafasi hiyo kikatiba baada ya mtangulizi wake, Dk John Magufuli kufariki dunia Machi 17, 2025.

Chini ya Falsafa ya Kazi Iendelee, Rais Samia amekuwa kinara wa utekelezaji kwa kasi miradi ya maendeleo iliyoachwa na mtangulizi wake na wakati huo huo akiibua mingine kwa ajili ya ustawi wa Watanzania.

Aidha, sifa yake kubwa ya kupenda amani inadhihirisha uhalali wa jina la Chifu Hangaya kutokana na kipindi chote cha kwanza cha uongozi kujipambanua kuwa kiongozi mwenye kutafuta suluhu ya mambo kwa majadiliano na maridhiano.

Tangu alipoingia madarakani mwaka 2021, ameonesha uongozi wa hekima na mazungumzo badala ya migongano. Mfano halisi ni hatua yake ya kukutana na viongozi wa vyama vya upinzani, ili kujenga maridhiano ya kisiasa na kurejesha imani ya wananchi katika siasa za kidemokrasia.

Kupitia Falsafa ya 4R (Maridhiano, Ustahimilivu, Mabadiliko na Kujenga upya), Rais Samia ameweka msingi wa Tanzania mpya inayotafuta umoja na maendeleo kwa maelewano huku falsafa ikijikita katika kuponya majeraha ya kisiasa, kijamii na kiuchumi kwa njia ya majadiliano na ushirikiano.

Ndani ya falsafa hiyo, Maridhiano yamekuwa mhimili mkuu wa kuunganisha makundi yote; Uvumilivu unaimarisha mshikamano; Mabadiliko yanahamasisha mageuzi ya taasisi; na Ujenzi upya unalenga kujenga taifa lenye misingi ya haki na ustawi.

Kwa falsafa hii, Rais Samia amethibitisha kuwa ni Chifu Hangaya; ambaye ni kiongozi wa hekima anayesimamia umoja, amani na maendeleo kwa misingi ya mazungumzo na maridhiano.

Pamoja na sifa nyingine, ndio msingi mkuu wa wananchi kuendelea kumpa ridhaa ya kuendelea kuongoza nchi kipindi cha pili kupitia uchaguzi wa kidemokrasia wa Oktoba 29, 2025.

### Wasifu wake

Kwa mujibu wa tovuti ya Ikulu, Rais Samia alizaliwa Januari 27, 1960 katika Kijiji cha Kizimkazi Mkoa wa Kusini Unguja katika upande wa pili wa Muungano, Zanzibar.

Alifunga ndoa na mtaalamu wa kilimo, Hafidh Ameir mwaka 1978 na kujaliwa watoto wanne, watatu wa kiume na mmoja wa kike.

Safari yake ya kielimu ilianza mwaka 1966 alipojiunga na Shule ya Msingi Chwaka iliyoko Unguja hadi mwaka 1968 kabla ya kuhamiaShule ya Msingi Ziwani mwaka 1970. Baadaye alihamia Shule ya Msingi Mahonda na kuhitimu mwaka 1972.

Mwaka 1973 alijunga na Shule ya Sekondari ya Ng'ambo kwa masomo ya kidato cha kwanza hadi cha tatu, na Shule ya Sekondari Lumumba alikohitimu kidato cha nne mwaka 1976.

Mwaka 1983 alipata Astashahada ya Mafunzo ya Takwimu kutoka Chuo cha



Uchumi, Zanzibar.

Baada ya kufanya kazi kwa kipindi kifupi katika Wizara ya Mipango na Maendeleo, mwaka 1983 hadi 1986 alijiunga na Chuo cha Maendeleo ya Uongozi Mzumbe (IDM) kwa masomo ya juu katika Utawala wa Umma.

Alipata mafunzo katika vyuo mbalimbali ikiwamo Chuo cha Utawala wa Umma Lahore, Pakistan mwaka 1987, Taasisi ya Eastern and Southern African Management Institute (ESAMI) 1991 na Taasisi ya Uongozi ya Hyderabad India mwaka 1998 kwa masomo ya utawala.

Baadaye alijiunga na Chuo Kikuu cha Manchester, Uingereza kwa masomo ya juu ya uchumi, na pia alipata Shahada ya Uzamili ya Maendeleo ya Jamii kupitia programu ya pamoja kati ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na Chuo Kikuu cha Southern New Hampshire, Marekani.

Uzoefu serikalini

Uzoefu wake katika kuitumikia serikali kwa nyadhifa mbalimbali ulianza mwaka 1987 akiwa Ofisa Mipango Rasilimali na Karani wa Masijala 1977 hadi 1983.

Mwaka 2014 chini ya Utawala wa Rais Jakaya Kikwete, Samia alipewa jukumu la kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge maalumu lililojadili Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiongozwa na Samuel Sitta, na kuandaa Rasimu ya Katiba mpya ya Tanzania.

Mwaka 2005 hadi 2010 alishika nafasi ya Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) na Waziri wa Kazi, Vijana, Ajira, Maendeleo ya Wanawake na Watoto katika SMZ mwaka 2000 hadi 2005.

Aidha, alishika nafasi ya Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Muungano na Mazingira mwaka 2010 hadi 2015.

Nyota yake ya kuelekea kushika madaraka ya juu katika Serikali ya Tanzania ilianza kung'aa mwaka 2015 alipoandika historia mpya ya maisha yake kwa kuwa mwanamke wa kwanza Tanzania kuwa Makamu wa Rais, njia iliyomfikisha katika kiti cha urais.

## Uzoefu ndani ya CCM

Nafasi zote za uongozi alizowahi kushika hazikutokea isivyo Bahati, bali kwa kuwa msingi wake ulijengwa katika uaminifu wake kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM) tangu alipojiunga na siasa na kuwa mwanachama rasmi Juni 10, 1987.

Mwaka 2000 aliingia katika siasa za uchaguzi katika nafasi ya Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar kupitia Viti Maalumu Wanawake, nafasi aliyoitumikia hadi mwaka 2010.

Katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010, aligombea na kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Jimbo la Makunduchi katika Mkoa wa Kusini Unguja.

Mwaka 2002 alichaguliwa kuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM na pia akateuliwa kuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM; nyadhifa ambazo ameendelea kuzifanyia kazi hadi leo.

Rais Samia ni Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM Taifa, Mkutano Mkuu wa CCM Mkoa wa Kusini Unguja; na alikuwa Mjumbe wa Kamati za Siasa Mkoa na Wilaya ya Kusini Unguja.

Kwa upande wa Jumuiya za CCM, Samia ni mwanachama wa Jumuiya ya Wanawake wa Tanzania (UWT) kuanzia mwaka 1996 hadi sasa. Ameshiriki katika kuandika Ilani ya Uchaguzi ya CCM mara nne mfululizo tangu mwaka 2005 hadi 2025.

## Uzoefu katika taasisi nyingine

Mwaka 2016, Samia aliteuliwa na aliyekuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Ban Ki Moon, kuwa Mjumbe wa Jopo la Umoja wa Mataifa kuhusu Uwezeshaji wa Wanawake Kiuchumi akiwakilisha Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika na kumaliza mwaka 2017.

Katika nafasi hiyo, aliwasilisha mambo 27 kwenye jopo hilo ambalo Serikali ya Tanzania ilibainisha kama hatua za kimkakati kwa ajili ya kuweka mfumo endelevu wa kufikia usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi.

Miongoni mwa matokeo ya kazi zake ni kusimamia uanzishwaji wa majukwaa ya uchumi ya wanawake nchini ili kuwaunganisha wanawake wafanyabiashara wadogo na wa kati kwenye masoko, hasa wanawake wanaoishi mipakani.

Kazi nyingine ni ya kuwaunganisha na mikopo nafuu na kuhimiza mafunzo ya ujasiriamali pamoja na kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuanzisha kampeni ya kuongeza uwajibikaji katika kupunguza vifo vya wajawazito na watoto, maarufu kama 'Jiongeze Tuwavushe Salama'.

Aidha, amefanya kazi na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) mwa-

*> Inaendelea Uk 7 >*

# Wasifu wa Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania



# Safari ya utumishi, kisiasa ya Dkt. Nchimbi hadi Umakamu wa Rais

*- Na Halima Mlacha -*

**BALOZI Dk Emmanuel Nchimbi ambaye kwa mara ya mwisho alikuwa Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), sasa ndiye Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutokana na Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 29, 2025.**

Dk Nchimbi ni kiongozi aliyelelewa katika misingi ya nidhamu, uadilifu na utumishi kwa taifa ambaye safari yake ya maisha na uongozi imejaa matukio ya kipekee yanayoonesha uthabiti wa fikra, uwezo wa kiuongozi na moyo wa uzalendo.

Hayo ni miongoni mwa mambo mengi yaliyomweka katika mstari wa mbele wa kizazi kipya cha viongozi wa Tanzania.

Alizaliwa Desemba 24, 1971 mkoani Mbeya na kukulia katika familia yenye maadili ya kitaifa na kiutumishi ya Mzee John Nchimbi.

Baba yake, Mzee Nchimbi ni askari mstaafu wa Jeshi la Polisi aliyefikia ngazi ya Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) na aliyewahi kuwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mtwara.

Zaidi ya utumishi wake katika Jeshi la Polisi, Mzee Nchimbi alikuwa mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM (NEC) kwa vipindi viwili kupitia kundi la majeshi na alishiriki katika shughuli za chama kwa bidii kabla ya kustaafu masuala ya kisiasa baada ya mfumo wa vyama vingi kuanzishwa.

Malezi hayo ya kijeshi na kisiasa yalichangia kumjenga Dk Nchimbi kuwa mtu mwenye nidhamu ya hali ya juu, anayeheshimu mamlaka na kuamini katika uamuzi wa pamoja.

Alipata elimu ya msingi mkoani Dar es Salaam katika Shule ya Msingi Oysterbay kati ya mwaka 1980 hadi 1986.

Kisha, akaendelea na masomo ya sekondari katika Shule ya Uru (1987–1989) na baadaye katika Shule ya Sekondari ya Sangu alikohitimu kidato cha nne mwaka 1990.

Elimu ya kidato cha tano na sita aliipata katika Shule ya Forest Hill, Mbeya kati ya mwaka 1991 hadi 1993.

Baada ya hapo, alijiunga na Chuo cha IDM Mzumbe (sasa ni Chuo Kikuu cha Mzumbe) ambako alipata Stashahada ya Juu ya Utawala mwaka 1997.

Ndani ya kipindi hicho akiwa mwanafunzi, kipaji chake cha uongozi kilianza kung'aa alipoteuliwa kuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM (NEC) mwaka huo huo wa 1997.

Mwaka uliofuata (1998), alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), nafasi iliyomfanya kuwa miongoni mwa viongozi vijana wenye ushawishi mkubwa ndani ya chama.

Baada ya hapo, Dk Nchimbi alifanya kazi katika Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kuanzia mwaka 1998 hadi 2003, kabla ya kuteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Bunda mwaka 2003.

Aliendelea na masomo ya juu na kuhitimu Shahada ya Uzamili (MBA) katika Chuo Kikuu cha Mzumbe mwaka 2003, akibobea katika masuala ya benki na fedha.

Mwaka 2011 alihitimu Shahada ya Uzamivu (PhD) katika uongozi na usimamizi wa umma katika chuo hicho hicho cha Mzumbe.

Safari ya kisiasa ya Dk Nchimbi ilianza rasmi mwaka 2005 alipogombea ubunge katika Jimbo la Songea Mjini kupitia CCM na kushinda kwa asilimia 67.6 dhidi ya mpinzani wake kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Edson Mbogoro.

Mwaka huo huo, Rais wa Serikali ya Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete alimteua kuwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo.

Alitumikia nafasi hiyo hadi Oktoba 2006 alipohamishiwa Wizara ya Kazi, Ajira na Vijana.

Kati ya mwaka 2008 na 2010 alihudumu akiwa Naibu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kisha akawa Waziri wa Habari, Utamaduni, Vijana na Michezo mwaka 2010 hadi Mei 2012 alipohamishiwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi alikohudumu hadi Desemba 2013.

Baada ya kuhitimu majukumu ya ubunge mwaka 2015, Dk Nchimbi aliteuliwa na Rais wa Awamu ya Tano, Dk John Magufuli kuwa Balozi wa Tanzania nchini Brazil kati ya



> Ameonesha uaminifu mkubwa kwa chama, serikali na wananchi. Ninamwamini, atakuwa mshirika mwema katika safari yetu ya kujenga Tanzania ya maendeleo, amani na heshima kwa wote
>
> Dkt. Nchimbi ana uwezo wa kujenga hoja, kuheshimu taratibu za kimataifa na kuwakilisha nchi kwa heshima kubwa. Uwezo wake wa kujenga maridhiano ni sifa adimu

> Safari ya kisiasa ya Dk Nchimbi ilianza rasmi mwaka 2005 alipogombea ubunge katika Jimbo la Songea Mjini kupitia CCM na kushinda kwa asilimia 67.6 dhidi ya mpinzani wake kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Edson Mbogoro.

2016 na 2021.

Katika utumishi wake akiwa balozi, Dk Nchimbi alifanikiwa kuimarisha uhusiano wa kiuchumi, kibiashara na kielimu na kijamii kwa ujumla baina ya Tanzania na Brazil.

Mwaka 2022 alihamishwa kituo na kuwa Balozi wa Tanzania nchini Misri alikotumikia hadi Agosti 2023.

Januari 15, 2024, aliteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa CCM. Alitumia vyema nafasi hiyo kuimarisha mfumo wa chama, nidhamu ya ndani na ushirikiano kati ya chama na serikali.

Kabla ya uteuzi wake, nafasi hiyo ilikuwa inashikiliwa na Daniel Chongolo aliyeomba kujiuzulu.

Januari 2025, Mwenyekiti wa CCM na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan alimpendekeza kuwa Mgombea Mwenza wa Urais kupitia CCM katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 29, 2025.

Pendekezo hilo liliungwa mkono kwa kauli moja na wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM uliofanyika Januari 19, 2025.

Dk Nchimbi ameapishwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika tukio hilo la Novemba 3, 2025 lililofanyika Dodoma, Dk Nchimbi anarithi nafasi ya Dk Philip Mpango.

Katika hotuba yake ya kumtambulisha rasmi, Rais Samia anasema Dk Nchimbi ni kiongozi mwenye maono, nidhamu na uchapakazi wa hali ya juu.

"Ameonesha uaminifu mkubwa kwa chama, serikali na wananchi. Ninamwamini, atakuwa mshirika mwema katika safari yetu ya kujenga Tanzania ya maendeleo, amani na heshima kwa wote," anasema Rais Samia.

Dk Mpango anamwelezea Dk Nchimbi kama kiongozi kijana mwenye uwezo wa kipekee wa kusimamia masuala ya kiuchumi na kijamii.

"Anayo akili pana, anajua kuongoza watu na ni msikilizaji mzuri. Uteuzi wake unaonesha kuwa nchi yetu inaendelea kuwa na kizazi kipya cha viongozi wenye dira na maadili," anasema Dk Mpango.

Aliyewahi kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Profesa Palamagamba Kabudi anasema Dk Nchimbi ni mwanadiplomasia wa asili.

Anasema ana uwezo wa kujenga hoja, kuheshimu taratibu za kimataifa na kuwakilisha nchi kwa heshima kubwa. Uwezo wake wa kujenga maridhiano ni sifa adimu.

Waziri Mkuu mstaafu, Frederick Sumaye anasema Dk Nchimbi ni kiongozi mwenye nidhamu, anayejituma na mwenye moyo wa uzalendo.

Anasema, "Ni mfano wa viongozi wanaopanda kutokana na juhudi na si kwa bahati."

Dk Nchimbi na mkewe, Jane Nchimbi wamejaliwa kupata watoto watatu.

Safari ya Dk Nchimbi ni ushahidi kwamba uongozi bora hujengwa kwa misingi ya maadili, elimu na utumishi wa kweli kwa wananchi.

Kuanzia ngazi ya vijana, ubunge, uwaziri, ubalozi hadi makamu wa rais, ameonesha mfano bora wa kiongozi makini, mnyenyekevu na mwenye dira ya kitaifa.

# Wasifu wa Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi

Rais wa wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi



*- Na Khatib Suleiman -*

**Rais wa Zanzibar, Dk Hussein Mwinyi ameibuka na ushindi wa kishindo katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2025 baada ya kupata kura 448,892 sawa na asilimia 74.80.**

Mshindani wake wa karibu, Othman Masoud Othman wa Chama cha ACT-Wazalendo alipata kura 139,399 sawa na asilimia 23.22.

Dk Mwinyi ameapa na kuanza rasmi kuwatumikia Wazanzibar kwa kipindi kingine cha miaka mitano tangu 2025 hadi 20230. Kwa mara ya kwanza, Dk Mwinyi alichaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar kupitia Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

Ushindi wa Dk Mwinyi unampa nafasi zaidi kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2025-2030 katika maeneo mbalimbali muhimu ikiwemo masuala ya ajira kwa kundi la vijana pamoja na maendeleo ya kijamii.

Yapo mambo kadhaa yaliyombeba Dk Mwinyi na kuwa karata muhimu kumwezesha kushinda kwa kishindo katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 29,2025.

## Mambo 'yaliyombeba' Mwinyi Uchaguzi 2025

Uchunguzi kupitia vyanzo mbalimbali unabainisha kuwa, utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2020-2025 ni miongoni mwa mambo makubwa yaliyomwezesha Dk Mwinyi kupata ushindi wa kishindo.

Inaelezwa kuwa, kwa kiasi kikubwa Dk Mwinyi amefanikisha ilani hiyo katika maeneo yote muhimu yakiwemo ya maendeleo, kiuchumi na kijamii.

Mwaka 2020 alipochaguliwa kuiongoza Zanzibar, Dk Mwinyi alisema anakusudia kuwaunganisha Wazanzibari kuwa kitu kimoja.

Alipania Mwinyi alipania na kufanikiwa kuondoa ubaguzi na mifarakano iliyojengeka na kuota mizizi ya Upemba na Uunguja pamoja na Kaskazini na Kusini na hata kuondoa tofauti za kisiasa zilizotawaliwa na vyama vya siasa vya CCM pamoja na ACT-Wazalendo.

Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM na mwanasiasa mkongwe wa Zanzibar, Mohamed Aboud anasema: "... tofauti za kisiasa zilizokuwepo awali kwa kiasi kikubwa zimetoweka moja kwa moja kwani ilifika wakati watu hawazikani kwa sababu ya tofauti ya vyama vya siasa."

Ushindi wa Mwinyi kwa kiasi kikubwa umebebwa pia na mafanikio katika utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Mwaka 2020-2025 kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya kijamii.

Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa hospitali 11 za wilaya Unguja na Pemba pamoja na hospitali kubwa ya mkoa iliyopo Lumumba Unguja.

Hili lilitokana na matamanio yake ya kuhakikisha wananchi Zanzibar wanapata huduma bora za afya zikiwemo za matibabu ya kibingwa wakiwa nchini bila kulazimika kwenda nje ya nchi.

Katika kipindi cha kwanza cha urais wake Zanzibar, kwa mara ya kwanza huduma za matibabu ya magonjwa ya figo zimeanza kutolewa Zanzibar, hivyo wagonjwa waliokuwa wakisumbuliwa na matatizo hayo hawana sababu ya kusafirishwa kwenda Tanzania Bara.

Katika kipindi hicho , zaidi ya mashine nane za kusafisha figo zimefungwa katika Hospitali ya Lumumba Unguja zikitoa matibabu hayo bure.

Kwa takribani miaka mitatu sasa, wagonjwa 60 wamepata huduma hizo ambazo zimefikishwa hadi katika hospitali za Pemba ikiwemo ya Abdallah Mzee.

Katika elimu, Dk Mwinyi katika kipindi cha kwanza cha uongozi amejenga shule 32 za ghorofa kwa ajili ya wanafunzi wa shule za msingi na sekondari Unguja na Pemba kwa lengo la kupunguza msongamano kwa wanafunzi katika madarasa.

Awali, wanafunzi walikuwa wakisoma zaidi ya 100 kwa wakati mmoja. Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Khamis Abdalla Said anasema Dk Mwinyi amekuja na baraka kubwa za kutekeleza miradi mingi katika sekta ya elimu.

Anasema hii ni pamoja na kuimarisha vyuo vya amali ili kuzalisha ajira nyingi kwa vijana na kuwafanya kuwa wajasiriamali.

Anasema katika Mwaka wa Fedha 2025 /2026, wizara inakusudia kujenga vyuo vya amali vitano Unguja na Pemba.

Vyuo hivyo vitawawezesha wahitimu kuingia katika soko la ajira huku wakiboresha mfumo wa masomo kwa kuongeza masomo yatakayowaingiza katika soko la ajira moja kwa moja.

"Sekta ya elimu katika kipindi cha miaka mitano imepiga hatua kubwa ikiwemo kuongeza idadi ya ufaulu kwa wanafunzi kuingia kidato cha tano na sita hadi vyuo vikuu nchini," anasema.



# Chifu Hangaya, kinara wa kasi ya maendeleo



*> Inatoka Uk 3 >*

ka 1988 hadi 1997. Amefanya kazi katika kamati, bodi na taasisi mbalimbali ikiwamo Kamati ya Msamaha wa Wafungwa ya Zanzibar mwaka 2001 hadi 2010 na Mlezi wa Jumuiya ya Watu Wanaoishi na Virusi vya Ukimwi Zanzibar 1997 hadi 2000.

Amekuwa Mjumbe wa Bodi ya Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote (EOTF) 1996 hadi 2000 na Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Taasisi zisizo za Kiserikali Zanzibar (ANGOZA) 1995 hadi 2000.

Kwa mujibu wa vyanzo mbalimbali, pia amewahi kuwa mwanachama wa Lions Club Zanzibar 1991 hadi 1998, Mjumbe wa Kamati ya Uundaji wa Sera ya Elimu Zanzibar 1996 na Mwanachama Mwanzilishi wa Taasisi ya Kuchochea Maendeleo ya Wanawake Zanzibar 1991 hadi 1994.

Rais Samia aliingia madarakani nchi ikiwa katika kipindi kigumu kiuchumi huku dunia ikitetereshwa na ugonjwa wa virusi vya korona (Covid-19).

Tangu aingie madarakani, amehakikisha anatekeleza miradi yote mikubwa na ya kimkakati iliyoanzishwa na mtangulizi wake (Magufuli), si tu kuitekeleza bali pia kuikamilisha kwa wakati sambamba na kuidhinisha mingine mipya.

Mambo mengine aliyoyafanya ni kuinua sekta ya utalii akiwa mwongoza watalii namba moja kupitia Filamu ya 'Tanzania: The Royal Tour' iliyotayarishwa na Mmarekani Peter Greenberg mwaka 2021.

Filamu hiyo imetoa mchango mkubwa katika kuongeza idadi ya watalii wanaoingia nchini kwa zaidi ya asilimia 100.

Anatambulika kuwa kinara wa diplomasia ya uchumi aliyefanikiwa kuiunganisha Tanzania na mataifa mengine ya Afrika na dunia kibiashara na kidiplomasia.

Ziara zake duniani hazikuwa za bure kwani zimekuwa zikizaa matunda yaliyopaisha uchumi wa Tanzania kupitia sekta mbalimbali za kimkakati zikiwamo za madini, bandari na usafirishaji.

Mwaka 2022 Jarida la Marekani la Time lilimtaja Rais Samia kuwa miongoni mwa watu 100 wenye ushawishi mkubwa zaidi duniani.

## Tuzo

Miongoni mwa tuzo alizotunukiwa ni pamoja na Tuzo ya Africa Road Builders ya Babacar Ndiaye mwaka 2022 na mwaka huo huo akapewa Tuzo ya Uongozi Uliokubalika inayotolewa na Taasisi ya CARE International.

Aidha, aliandikwa kwenye orodha ya Jarida la Forbes ya wanawake 100 wenye nguvu zaidi duniani.

Mbali na hizo, alipewa tuzo kadhaa za kitaaluma kutoka vyuo vikuu vya ndani na nje ya Tanzania ikiwamo Shahada ya Udaktari wa Heshima kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu cha Jawaharlal Nehru cha India; Chuo Kikuu cha Zanzibar, Chuo Kikuu cha Ankara, Uturuki, Chuo Kikuu cha Anga cha Korea Kusini na Chuo Kikuu cha Mzumbe. Huyu ndiye Samia; nyota inayoendelea kung'ara.



# Malengo nane ya Ofisi ya Msajili wa Hazina Kubadilisha taswira ya Mashirika ya Umma



**Dar es Salaam. Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina (OMH) imeweka malengo makubwa nane ya kimkakati yanayolenga kubadilisha sura ya mashirika ya umma nchini ifikapo mwaka 2030.**

Malengo hayo, yaliyoainishwa ndani ya Mpango wa Kimkakati wa Miaka Mitano wa OMH (2025/26–2029/30), yanalenga kuongeza mchango wa mashirika hayo katika uchumi wa taifa, kupunguza utegemezi wa ruzuku, na kuhakikisha uwekezaji wa umma unaleta tija kwa wananchi.

Hatua hii inachukuliwa katika kipindi ambacho Tanzania ipo kwenye safari ya mageuzi ya kiuchumi, ikiwa imeweka bayana kupitia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 kwamba inataka kuwa miongoni mwa mataifa matano yenye uchumi mkubwa zaidi Kusini mwa Jangwa la Sahara katika kipindi cha miaka 25 ijayo.

Kwa mujibu wa dira hiyo, Tanzania imepanga kufikia Pato la Taifa la takribani $1 trilioni ifikapo mwaka 2050 — ikimaanisha ukuaji wa wastani wa asilimia 10.3 kwa mwaka, kutoka thamani ya sasa ya takribani $85.98 bilioni.

Hilo linawezekana hasa kwa kuzingatia historia thabiti ya mafanikio ya muongo uliopita, kipindi ambacho Tanzania imeimarisha uchumi wake kwa karibu mara mbili na kudhihirisha uimara wa sekta za viwanda, kilimo, madini, utalii na huduma za kifedha.

Ni katika muktadha huo wa matumaini na uthabiti ambapo OMH imeandaa mpango huu wa kimkakati unaoelezwa kuwa "mwongozo wa mageuzi" ya mashirika ya umma ili yawe chachu ya uchumi wa kisasa unaotegemea uzalishaji, ufanisi na uwekezaji.

## Malengo makubwa ya kimkakati

Kati ya malengo hayo, OMH inalenga kuongeza mchango wa mashirika ya umma katika Pato la Taifa kutoka asilimia 5 hadi 10, huku mchango wa mapato yasiyo ya kodi kwenye mapato ya ndani ukiongezeka kutoka asilimia 3.6 hadi 5.

Vilevile, ofisi hiyo inapanga kuwa na Mfuko wa Uwekezaji wa Umma (Public Investment Fund) ambao thamani yake ifikapo mwaka 2030 inatarajiwa kuwa takribani $10 bilion, pamoja na kuongeza wastani wa faida ya mtaji (ROE) kutoka asilimia 5 hadi 10.

Malengo mengine ni kuhakikisha kuwa asilimia 100 ya mashirika ya umma yanaongeza mapato kila mwaka (kutoka asilimia 50 ya sasa), kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka asilimia 49 hadi 30, kuhakikisha asilimia 30 ya mashirika hayo yanajiendesha kwa faida, na kuchochea upatikanaji wa angalau $500 milioni kupitia mauzo ya nje ya mashirika ya umma.

"Tumejipanga kuhakikisha mashirika ya umma yanakuwa injini ya ukuaji wa uchumi wa taifa. Tunataka kuona uwekezaji wa umma ukibadilika kutoka umiliki wa kawaida hadi chanzo cha faida kwa Watanzania wote," alisema hivi karibuni Msajili wa Hazina, Bw. Nehemiah Mchechu.

## Malengo ya kimkakati ya miaka mitano

OMH imeanza safari ya mageuzi makubwa ili kubadilisha jinsi uwekezaji wa umma unavyosimamiwa, kuhamasishwa, na kutumika kwa ufanisi nchini Tanzania.

Mpango wa Kimkakati wa Miaka Mitano wa OMH unaweka malengo makubwa lakini yanayotekelezeka, yanayolenga kujibu changamoto muhimu za taasisi, mahitaji ya uchumi wa taifa, na fursa mpya za maendeleo.

Kupitia mpango huu, Ofisi hiyo imebainisha maeneo matano ya kipaumbele yatakayoongoza utekelezaji wake wa kimkakati: kuimarisha utawala bora na kuboresha uongozi na uendelezaji wa rasilimali watu.

Maeneo mengine ni kuongeza ufanisi katika usimamizi wa utendaji, kuimarisha uhamasishaji na utunzaji wa rasilimali, pamoja na kuboresha na kufafanua uwekezaji wa umma ili kuongeza tija na ushindani wa taifa kiuchumi.

Kila eneo limeandaliwa kupitia mchakato makini uliohusisha wadau, uchambuzi wa sekta, kulinganisha na

mbinu bora za kimataifa, na tafakari ya kina kuhusu nafasi ya mashirika ya umma katika uchumi wa karne ya 21.

## Kwa nini malengo haya ni muhimu

Uwekezaji wa umma nchini Tanzania una uwezo mkubwa wa kuleta mageuzi katika sekta muhimu kama nishati, miundombinu, kilimo, na teknolojia.

Hata hivyo, kwa miongo kadhaa changamoto za utendaji, upungufu wa mitaji, na utegemezi mkubwa kwa serikali zimekuwa kikwazo kikubwa.

Malengo ya kimkakati ya OMH yamekusudiwa kuondoa changamoto hiyo — yakihamisha dhana ya usimamizi wa mali za umma kutoka katika mfumo wa urasimu wa kiserikali kwenda katika usimamizi wa kitaalamu unaozalisha matokeo.

Haya ni mageuzi yanayolenga kuifanya Tanzania ijenge msingi wa uchumi unaojitegemea kupitia mashirika ya umma yenye tija na yanayoweza kuhimili ushindani wa soko.

## Uanzishaji wa Mfuko wa Uwekezaji wa Umma

Kupitia mpango huu, OMH inajielekeza katika kusimamia kwa ufanisi mashirika yote yenye umiliki wa serikali ili kuongeza mchango wake katika ukuaji wa uchumi na mapato ya ndani.

Lengo, alisema Bw. Mchechu, ni kuhakikisha mali za umma zinatumika kikamilifu na kuleta matokeo yanayoonekana kwa taifa.

Kupitia mfuko huo, serikali itapata fursa ya kuwekeza katika miradi yenye tija, kuongeza mapato, na kujenga misingi ya uchumi wa viwanda unaojitegemea — huku ikiimarisha uthabiti wa kifedha wa mashirika ya umma.

## Ujenzi wa mashirika yenye nguvu kifedha

OMH inalenga kuhakikisha kuwa mashirika ya umma yanajitegemea kifedha, yanafanya kazi kwa weledi, na yanazalisha faida.

Kwa mujibu wa mpango huo, asilimia 100 ya mashirika ya umma yatakuwa yakiongeza mapato kila mwaka, huku utegemezi wa ruzuku ukipungua kutoka asilimia 49 hadi 30.

Hii inaenda sambamba na kuongeza wastani wa faida ya mtaji kutoka asilimia 5 hadi kufikia asilimia 10, na kuhakikisha angalau asilimia 30 ya mashirika yanafanya kazi kwa faida ifikapo mwaka 2030.

> “Tumejipanga kuhakikisha mashirika ya umma yanakuwa injini ya ukuaji wa uchumi wa taifa. Tunataka kuona uwekezaji wa umma ukibadilika kutoka umiliki wa kawaida hadi chanzo cha faida kwa Watanzania wote

> “OMH inalenga kuhakikisha kuwa mashirika ya umma yanajitegemea kifedha, yanafanya kazi kwa weledi, na yanazalisha faida. Kwa mujibu wa mpango huo, asilimia 100 ya mashirika ya umma yatakuwa yakiongeza mapato kila mwaka, huku utegemezi wa ruzuku ukipungua kutoka asilimia 49 hadi 30

Hatua hizi zinalenga kujenga msingi wa mashirika yenye ufanisi, yanayowajibika, na yenye ushindani wa kimataifa — hasa katika mazingira ambapo soko la kikanda la Afrika Mashariki linaendelea kukua na ushindani unazidi kuongezeka.

## Kupanua wigo wa mapato ya kigeni

Katika dunia ya leo yenye ushindani mkubwa wa kibiashara, uwezo wa nchi kupata fedha za kigeni ni kipimo cha uthabiti wake wa kiuchumi.

Ndiyo maana OMH inapanua wigo wa mashirika ya umma hadi katika masoko ya kimataifa ili kuhakikisha mashirika haya yanachangia angalau $500 milioni kupitia mauzo ya nje.

Hatua hii itaimarisha upatikanaji wa fedha za kigeni, kusaidia kudhibiti nakisi ya biashara, na kuongeza thamani ya Shilingi ya Tanzania.

## Wito

OMH inasisitiza kuwa mafanikio ya mpango huu yatategemea ushirikiano wa wadau wote—kutoka kwa viongozi wa mashirika ya umma, sekta binafsi hadi wananchi.

“Hii ni safari ya pamoja ya kubadilisha thamani ya mali za umma kuwa utajiri wa taifa. Tunahitaji uwajibikaji, ufanisi na uwazi katika kila hatua,” alisisitiza Bw. Mchechu.

Kadri Tanzania inavyoelekea kufikia Dira ya 2050, mpango huu wa kimkakati wa OMH unakuwa dira ya mabadiliko ya kweli—ukilenga kuibua fursa mpya za uwekezaji, kuongeza mapato, na kuboresha maisha ya wananchi kupitia usimamizi bora wa mali za umma.



# SALAMU ZA PONGEZI



Menejimenti, na Watumishi wa STAMICO tunatoa salamu za pongezi kwa **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

STAMICO, kwa heshima kubwa tunaahidi kutekeleza maono yako katika sekta ya Madini na pia katika kuhamasisha matumizi ya Nishati Safi huku tukiunga mkono juhudi zote za Serikali yako katika kuleta maendeleo jumuishi na endelevu kwa Watanzania wote.



Menejimenti, na Watumishi wa STAMICO tunatoa salamu za pongezi kwa **Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi** kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

STAMICO, kwa heshima kubwa tunaahidi kutoa ushirikiano wa dhati kwa Ofisi ya Makamu wa Rais katika kulinda mazingira yetu na kuunga mkono juhudi zote za Serikali ya Awamu ya Sita katika kuleta maendeleo jumuishi na endelevu kwa Watanzania kupitia Sekta ya Madini.



Menejimenti, na Watumishi wa STAMICO tunatoa salamu za pongezi kwa **Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi** kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

STAMICO, kwa heshima kubwa tunaahidi kutoa Ushirikiano wa dhati kuunga mkono juhudi za Serikali yako katika kujenga mahusiano mazuri ya ki Muungano na yanayoleta maendeleo jumuishi na endelevu kwa Watanzania kupitia Sekta ya Madini.

# Pongezi za STAMICO kwa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutambua mchango wake katika kujenga Uchumi wa Madini endelevu kuelekea Dira 2050

**Menejimenti na Watumishi wote wa Shirika la Madini Tanzania (STAMICO) tunapenda kutoa salamu za pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ushindi mkubwa na wa kihistoria katika Uchaguzi Mkuu wa 2025. Ushindi huu ni ishara ya imani kubwa ya Watanzania waliyo nayo kutokana na uongozi wako thabiti.**

Chini ya uongozi wako, Sekta ya Madini imepiga hatua kubwa katika mageuzi, uwazi, na ushirikishwaji wa Watanzania. Wachimbaji wadogo na hususani wale walio katika makundi maalumu ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, yamepata nafasi kubwa ya ushirikishwaji na pia kuwezeshwa kwa kupatiwa vifaa vya kisasa vya utafiti na uchorongaji. Jambo hili limekuwa mfano wa kuigwa na hata kwa nchi majirani na Tanzania.

STAMICO inajivunia kuwa sehemu ya mafanikio hayo na itaendelea kushirikiana na Serikali katika kuhakikisha Sekta ya Madini inakuwa kichocheo cha maendeleo endelevu. Tunakuombea afya njema, hekima, na nguvu za kuendeleza kazi kubwa ya kuijenga Tanzania yenye uchumi imara, jumuishi na unaotazama mustakabali wa kizazi kijacho.

Tunakuahidi kuendelea kutekeleza kwa vitendo maono yako katika Sekta ya Madini na kuendelea kufanya kazi kwa ufanisi ili kulifanya Shirika hili la Madini la Taifa ambalo ni Shirika kongwe kuendelea kuwa la mfano.

### Historia ya STAMICO

Shirika la Madini Tanzania (STAMICO) lilianzishwa mwaka 1972 kwa lengo la kushiriki moja kwa moja katika shughuli za utafiti, uchimbaji, usafishaji, biashara, na uwekezaji katika Sekta ya Madini kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.


Baada ya mabadiliko ya kiuchumi na kisera yaliyolenga kukuza ushiriki wa Sekta binafsi katika uchumi, STAMICO ilirejeshwa upya mwaka 2010 ikiwa na dhamira ya kuhakikisha Watanzania wananufaika zaidi na utajiri wa madini uliopo nchini.

### Mchango wa STAMICO katika uchumi wa madini

Katika kipindi cha Uongozi wa Awamu ya Sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, STAMICO imekuwa mstari wa mbele katika kuimarisha mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa, ambalo limeongezeka kutoka wastani wa asilimia 3.5 mwaka 2015 hadi zaidi ya asilimia 10 mwaka 2024. Hii ni matokeo ya usimamizi bora, sera thabiti, na uwekezaji unaoongozwa na uelewa wa kina wa fursa zilizopo.

### Uwekezaji wa moja kwa moja na ule wa ubia kwenye miradi ya kimkakati

STAMICO, imewekeza katika miradi ambayo ina umiliki wa asilimia mia moja (100%) na pia ambayo imeingia ubia na kampuni za watu binafsi. Kupitia miradi kama ya Makaa ya Mawe wa Kiwira (Songwe), Mradi wa Kokoto wa Chigongwe (Dodoma) na ile yenye ubia na makampuni binafsi mfano



***Dkt. Venance Mwasse***
*Mkurugenzi Mtendaji wa STAMICO*

mradi mkubwa wa kuichenjua na kuisafisha dhahabu wa Mwanza kwa kushirikiana na kampuni ya Mwanza Precious Refinery Metal, mradi wa kuchimba dhahabu kule Geita kwa kushirikiana na Kampuni ya Buckreef Gold Mine na mradi wa kuchimba dhahabu Biharamulo kupitia kampuni yake tanzu ya STAMIGOLD , Shirika limechangia katika kuongeza uzalishaji wa madini hivyo kuchangia katika kuongeza pato la taifa.

### Matumizi ya Teknolojia na utafiti wa Kijiofizikia

Chini ya Serikali ya Awamu ya Sita, Shirika limeweza kununua mitambo 15 ya uchorongaji pamoja na vifaa vya kisasa vya utafiti wa kijiofizikia (Geophysical Surveys Equipments) vinavyowezesha wachimbaji kujua kwa usahihi maeneo ambayo madini yapo.

Hii imechangia katika kuvutia wawekezaji na kuongeza mapato ya Serikali kupitia leseni za utafiti na uchimbaji. Shirika pia limetumia baadhi ya kampuni ambazo zina uwezo wa kufanya utafiti wa kina kutumia ndege maalumu katika maeneo ambayo Shirika limepewa leseni za madini mbalimbali.

Aidha, STAMICO imeendelea kutumia vituo vyake vya mfano vya kuchenjua dhahabu vya Lwamgasa, Katente na Itumbi, katika kuwasaidia wachimbaji wadogo kuongeza thamani ya madini kama ambavyo sheria ya madini inaelekeza.

Vituo hivi vimesaidia kusogeza matumizi ya teknolojia kwa wachimbaji wadogo, kupunguza upotevu wa mapato ya Serikali na kuongeza mchango wa Sekta katika ajira kwa wachimbaji wadogo hususan makundi maalumu ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

### Matumizi ya Nishati Safi na kuongeza thamani kwenye Madini

STAMICO imeendelea kuienzi kwa vitendo ajenda ya Serikali ya Awamu ya Sita kuhusiana na matumizi ya Nishati safi. Nishati hii ambayo imetokana na ubunifu mkubwa uliofanywa na Shirika wa kuyaongezea thamani makinikia ya Makaa ya Mawe kupitia mchakato wa kiwandani, uliolenga kupunguza hewa ya ukaa na kuzalisha Nishati safi na salama ya kupikia inayojulikana kwa jina la Rafiki Briquettes.

Nishati hii pia hutumika katika kukaushia mazao na pia kuendehsa mitambo mbalimbali. Shirika limeweza kujenga viwanda vitatu vya uzalishaji wa Nishati hii katika Mikoa ya Dar es salaam, Pwani na Songwe ambavyo vinafanya kazi. Tayari Shirika lipo katka hatua za mwisho za kufunga viwanda vingine viwili katika Mikoa ya Dodoma na Tabora. Shirika pia limepanga kufunga viwanda vingine viwili katika Mikoa ya Tanga na Geita. Viwanda hivi pamoja na mtandao mzuri wa usambazaji ambao STAMICO imeutengeneza kupitia mawakala, utasaidia kumtua Mama kuni lakini kuhakikisha Nishati hii inasambaa Tanzania nzima. STAMICO imejipanga kuyaenzi na kuyaishi Maono ya Mheshimia Rais Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha kwamba mpaka inapofika mwaka 2034, Watanzania zaidi ya asilimia 80 wawe wanatumia Nishati Safi.

### STAMICO na Dira 2050

Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 inalenga kujenga Tanzania yenye uchumi wa kati wa juu, wenye viwanda imara, watu walioelimika, na miundombinu ya kisasa.

Kupitia mikakati yake ya muda mfupi na mrefu, STAMICO imejipanga kuchangia katika maeneo yafuatayo:

- Kuchochea viwanda vya ndani kwa kuzalisha malighafi zinazotumika katika utengenezaji wa bidhaa za chuma, umeme, vito na kemikali.
- Kuwezesha wananchi kiuchumi kwa kuanzisha vituo vya mfano vya wachimbaji wadogo na programu za mafunzo ya uchimbaji salama na endelevu.
- Kukuza mapato ya Serikali kupitia uwekezaji wa kimkakati na ubia wenye tija. Kuhifadhi mazingira kwa kuhakikisha shughuli zote za uchimbaji zinafuata viwango vya kimataifa vya usimamizi wa mazingira.

### Maono ya STAMICO kwa mustakabali wa Sekta ya Madini

STAMICO inalenga kuongeza uwekezaji wake katika miradi ya kimkakati, hususani madini muhimu kama vile nikeli, grafiti, chuma, urani, shaba, na lithium. Haya ni madini ambayo ni muhimu kwa teknolojia za kisasa kama magari ya umeme na nishati jadidifu.

Hatua hii inaendana na jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita katika kujenga uchumi wa kisasa unaozingatia mazingira na mabadiliko ya teknolojia duniani.

Zaidi ya hapo, STAMICO inaendelea kutekeleza mkakati unaolenga kuhakikisha rasilimali za madini zinachangia moja kwa moja katika ustawi wa wananchi kupitia ajira, huduma za kijamii, na miundombinu inayojengwa katika maeneo ya migodi.

**WIZARA YA NISHATI**
**WAKALA WA NISHATI VIJIJINI (REA)**

Rural Energy Agency
REA
TANZANIA
Energising Rural Transformation

# HONGERA

Bodi ya Nishati Vijijini (REB), Menejimenti na Watumishi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) tunakupongeza Mheshimiwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Tunaahidi kuendelea kutekeleza kwa vitendo, maono na maelekezo yako ya kuhakikisha Wananchi wa vijijini wanapata huduma bora za Nishati.



Bodi ya Nishati Vijijini (REB), Menejimenti na Watumishi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) tunakupongeza Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi kwa kuapishwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.



Tangazo hili limetolewa na:
Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA)

wakalawanishativijijini_rea
Wanishati
www.rea.go.tz

PPRA
Public Procurement Regulatory Authority

# PONGEZI

**Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania



**Tunakupongeza Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan** kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi cha pili cha Awamu ya Sita.

PPRA tunaahidi kufanya kazi kwa Juhudi, Ufanisi na Ubunifu katika kusimamia Ununuzi wa Umma.

## PPRA yajivunia uongozi wa Rais Samia

Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan amethibitisha kwa vitendo maono ya kuijenga Tanzania yenye maendeleo ya watu, miradi, uwajibikaji, uadilifu na matumizi bora ya rasilimali za umma; ambavyo kwa asilimia kubwa vimetekelezwa kupitia Ununuzi wa Umma.

Katika kipindi chake cha miaka minne, amefanikisha kuwa na Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023, iliyowapa fursa nyingi Watanzania. Pia, alijenga Mfumo wa Ununuzi wa Umma Kielektroniki (NeST) ambao umeongeza uwazi, uwajibikaji na haki kwenye michakato ya ununuzi wa umma.

**SHERIA YA UNUNUZI WA UMMA YA MWAKA 2023:**

- Imeelekeza zabuni zenye thamani ya hadi ***Shilingi Bilioni 50*** kutengwa kwaajili ya wazabuni watanzania pekee;
- Taasisi kutenga asilimia 30 ya bajeti ya ununuzi kwaajili ya makundi maalum (wanawake, wazee, vijana na watu wenye ulemavu. Hatua iliyoongeza ajira kwa maelfu ya Watanzania;
- Imeweka upendeleo wa asilimia 15 kwa bidhaa na huduma zinazozalishwa ndani ya Tanzania;
- Serikali imeokoa takribani Shilingi bilioni 13.3 kutokana na kupungua kwa matumizi ya karatasi na wino;
- Serikali kupunguza uzalishaji wa hewa ya ukaa ($CO_2e$) kwa kiasi cha tani 617.85 kwa mwaka 2023/2024;
- Imetaka kila ununuzi wa umma kufanyika ndani ya Mfumo wa NeST.

**MAFANIKIO BAADA YA KUTUMIKA KWA NeST (JULAI 2023 – OKTOBA 2025):**

- NeST imeunganishwa na Mifumo zaidi ya 20 ya Serikali;
- Imesaidia kupata taarifa sahihi kwani inasomana na mifumo 20;
- Makundi maalum yamepata zabuni zenye thamani ya zaidi ya ***Shilingi Bilioni 24*** (Julai 2023 - Oktoba 2025);
- Uzingatiaji wa Sheria ya Ununuzi uliongezeka kwa asilimia 10.4 kutoka asilimia 65.1 mwaka 2024 hadi kufikia asilimia 75.5;
- Imesaidia kuwa na taarifa sahihi;
- Imepunguza muda na gharama za zabuni; kuongeza ufanisi, uwajibikaji na usawa;
- Ongezeko la kasi ya ukamilishwaji wa miradi;
- Ufuatiliaji wa ununuzi umekuwa rahisi zaidi na wenye ufanisi zaidi.

**TUNAMTAKIA KILA LA HERI, TUNAAHIDI KUFANYA KAZI KWA JUHUDI, UADILIFU NA UFANISI ILI KUTIMIZA MAONO YAKE MEMA KWA TAIFA LETU.**

PPRA TANZANIA ppra_tanzania

*Tunakuahidi Ushirikiano wakati wote wa Uongozi wako*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TIB DEVELOPMENT BANK
Your Partner for Growth

# BENKI YA MAENDELEO TIB YAMPONGEZA MHESHIMIWA RAIS Dkt. SAMIA SULUHU HASSAN NA KUAHIDI KUENDELEZA USHIRIKIANO KATIKA UTEKELEZAJI WA MIPANGO YA SERIKALI ITAKAYOLETA MAENDELEO KWA WANANCHI



Benki ya Maendeleo TIB inatoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa ushindi wake mkubwa na kuchaguliwa kuendelea kuliongoza taifa letu tukufu la Tanzania.

Benki ya Maendeleo TIB kama taasisi ya fedha za maendeleo na benki ya kisera, inathibitisha dhamira yake ya kushirikiana na Serikali mpya katika kutekeleza mipango na vipaumbele vya maendeleo ya taifa kwa kutafsiri Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 pamoja na Ilani ya CCM 2025–2030 kuwa matokeo halisi yatakayoleta na kuchagiza maendeleo kwa Watanzania na Taifa kwa ujumla.

"Huu ni wakati wa matumaini mapya na dhamira ya kitaifa. TIB iko tayari kushirikiana kwa karibu na Serikali kufadhili miradi ya mageuzi inayochochea ukuaji wa viwanda, ajira, na ukuaji jumuishi wa uchumi," alisema Bw. Deogratius Kwiyukwa, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo TIB.

## Kutekeleza Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050

Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050, inalenga kuibadilisha nchi kuwa ya uchumi wa kipato cha kati unaotegemea viwanda na maendeleo ya watu. Dira hii inasisitiza jamii yenye uzalishaji, ubunifu, usawa na maadili ambayo haya yote ni kiini cha majukumu ya TIB.

Vilevile, Ilani ya CCM 2025–2030 inatilia mkazo kuongeza kasi ya ukuaji wa pato la Taifa kwa wastani wa asilimia 7, kuimarisha kilimo, kuongeza thamani ya mazao, kuwawezesha vijana, na kuunda ajira endelevu, maeneo ambayo benki ina uzoefu nayo na yapo katika mpango mkakati wake.

## Mchango wa TIB katika Ajenda ya Serikali Mpya:

### Uzalishaji Viwandani na Uongezaji Thamani:

TIB itaongeza ufadhili wa muda wa kati na mrefu kwa miradi ya uzalishaji, uchakataji wa mazao ya kilimo, na uongezaji thamani wa madini na bidhaa nyingine, ili kuongeza mauzo nje na kupunguza utegemezi wa bidhaa ghafi.

Kupitia ufadhili wa miradi ya miundombinu kama mitambo ya viwanda, nishati jadidifu, nishati ya umeme, miradi ya maji, na korido za usafirishaji, benki itasaidia kuondoa vikwazo vinavyopunguza tija na kuunganisha nchi kiuchumi.

### Mageuzi ya Kilimo

Kwa kuzingatia mkazo wa Ilani juu ya kilimo kama uti wa mgongo wa uchumi, benki kupitia dirisha la kilimo, itaendelea kufadhili miradi ya kilimo kwa riba nafuu ya asilimia 5 kwa mwaka. Fedha zitaelekezwa kwenye kilimo cha umwagiliaji, matumizi ya teknolojia za kisasa, maghala ya kuhifadhia mazao, na miradi ya masoko ili kuongeza kipato cha wakulima Tanzania nzima.

### Uwezeshaji Vijana na Wajasiriamali Wadogo (MSMEs)

Benki itaendelea kuongeza madirisha ya kifedha kwa miradi inayoongozwa na vijana, wanawake, na wafanyabiashara ndogo ndogo, ikihamasisha ajira na ujasiriamali katika kanda zote. Kama Benki ya Maendeleo, kwakushirikiana na wadau na taasisi za fedha za kimataifa benki itaendelea kuwezesha makundi haya muhimu ili waendelee kukuza mitaji yao kwa kupata mikopo yenye riba nafuu ili kuchochea ukuaji wa Uchumi jumuishi nchini.

### Miradi endelevu na utunzaji wa mazingira

TIB itatumia fursa za fedha za kijani na zenye masharti nafuu kufadhili miradi ya nishati jadidifu, kilimo endelevu, na miundombinu inayostahimili mabadiliko ya tabianchi.

"Wajibu wetu ni kuhakikisha kila shilingi inayowekezwa inachangia moja kwa moja ustawi na uimara wa Taifa letu la Tanzania," alisisitiza Bw. Kwiyukwa.

### Ushirikiano na Taasisi mbalimbali katika Maendeleo

TIB inakaribisha wizara, mamlaka za mikoa, sekta binafsi, na taasisi za maendeleo kushirikiana kufanikisha dira ya pamoja ya ustawi wa taifa. Hili litafanikiwa kwa kuwa na miradi yenye ubunifu katika uwekezaji, kujenga uwezo wa wataalamu, na mifumo ya ushirikiano kati ya taasisi na taasisi, TIB imejipanga kuwa kichocheo cha ukuaji jumuishi.

Tanzania inapoanza sura hii mpya ya uongozi, TIB inabaki imara katika dhamira yake ya kuwa injini ya kifedha ya mageuzi ya nchi, ikichochea maendeleo na kuwawezesha wananchi kufikia malengo ili kutimiza malengo ya Dira ya 2050.

"Tukishirikiana na Serikali mpya, Benki ya Maendeleo TIB tutaendelea kukuza ushirikiano na utekelezaji wa mipango itakayoleta na kuchagiza maendeleo kwa Watanzania na Taifa letu kwa ujumla tukilenga , kujenga Tanzania imara, jumuishi, na yenye mafanikio," alisisitiza Mkurugenzi Mtendaji.

***BENKI YA MAENDELEO TIB***
***— "Mshirika Wako Katika Maendeleo"***

tibdevelopmentbank

WCF
Workers Compensation Fund
ISO 9001 : 2015 CERTIFIED

# Salamu za PONGEZI



Bodi ya Wadhamini, Menejimenti na Watumishi wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), tunatoa Salamu za Pongezi kwa **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na **Mhe. Dkt. Emmanuel John Nchimbi** kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunawatakia kila lakheri katika utekelezaji wa majukumu.

***"Kazi na Utu, Tunasonga Mbele"***

# Dira 2050 na utekelezaji wake

Na Ikunda Erick

JULAI 17, mwaka huu Rais Samia Suluhu Hassan alizindua Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ambayo ni mwongozo wa kimkakati unaoelekeza Tanzania kufikia maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kiutamaduni ifikapo mwaka 2050.

Dira hiyo mpya ina maeneo manne ya kipaumbele ambayo ni Utawala Bora na Haki, Serikali za Mitaa Imara na Zenye Ufanisi, Utumishi wa Umma Unaowajibika na Amani, Usalama na Utulivu.

Dira inayoisha ina maeneo ya kipaumbele ambayo ni Kilimo cha Kisasa, Viwanda, Miundombinu na Teknolojia.

Utekelezaji wa Dira ya 2050 utaanza rasmi Julai 2026. Hii ni dira inayoonesha ndoto ya taifa kuwa nchi yenye uchumi imara, jumuishi na shindani duniani, huku wananchi wake wakifurahia ustawi, amani na heshima ya kimataifa.

Hata hivyo, mafanikio ya dira hii hayataletwa na serikali pekee, bali yanahitaji ushiriki wa kila Mtanzania, kuanzia ngazi ya familia hadi taifa.

Samia anakuwa Rais wa pili wa Tanzania kuandaa Dira ya Taifa ya Maendeleo, akitanguliwa na Rais wa Serikali ya Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa.

Dira hii imetokana na mchakato mrefu ambao Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, Dk Tausi Kida anasema Desemba 9, mwaka 2023 Rais Samia alizindua mchakato wa kukusanya maoni kutoka kwenye makundi mbalimbali yaliyojumuishwa kwenye dira hiyo.

Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, Dk Fredy Msemwa anasema zaidi ya watu 1,174,000 walitoa maoni ana kwa ana kwenye kaya zao ambayo yamejumuishwa ndani ya Dira ya 2050.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo anabainisha kuwa, mchakato wa maandalizi ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 ulishirikisha makundi yote ya jamii kwa kutumia njia zote za analojia na kidijiti.

Anasema asilimia 81 ya watu 1,132,837 waliojitokeza kutoa maoni yao kwa njia ya simu, tovuti na mitandao ya kijamii ni vijana wenye umri wa miaka 15 hadi 35.

"Hii inaakisi demokrasia ya nchi yetu. Kwa sasa, asilimia 76 ya Watanzania wote wapo chini ya miaka 36, kwa kuzingatia maoni hayo dira hii imeandikwa na vijana ambao wataishi nayo kwa muda mrefu zaidi," anasema Profesa Mkumbo.

Hata hivyo, dira inayotekelezwa sasa ilianza kutumika mwaka 2000 na itafikia ukomo wake Juni 30,2026.

Sasa Dira ya 2050 inaongozwa na misingi sita na msingi wake mkuu ni maendeleo ya watu yanayochochewa na uchumi imara, wenye ushindani na kipato cha juu ili kuinua viwango vya maisha ya wananchi na kuondoa umasikini.

Dira ya 2050 ina shabaha tatu ambazo ni kuiwezesha nchi kuwa ya kipato cha kati ngazi ya juu, ya uchumi wa viwanda, ikiwa na Pato la Taifa la Dola za Marekani trilioni moja na wastani wa pato la mtu mmoja la Dola za Marekani 7,000 kwa mwaka.

Msingi mwingine ni kutokomeza umasikini uliokithiri kwa makundi yote na Tanzania kuwa mzalishaji mkuu wa chakula barani Afrika na miongoni mwa nchi 10 bora duniani.

Kimsingi, dira hiyo si ya serikali peke, bali ni mali ya kila mwananchi. Inahimiza ushirikiano mpana, ikitambua kuwa maendeleo ya kweli hujengwa kwa nguvu ya pamoja.

Wanawake, vijana na nguvukazi yenye ujuzi ni rasilimali ya kipekee yenye uwezo wa kuleta mabadiliko makubwa, ikiongozwa na mtazamo sahihi, ubunifu na uthubutu.

Nguvukazi hiyo itakabiliana na changamoto zozote na kutumia fursa zinazojitokeza zikichagizwa na maendeleo ya kiteknolojia. Kwa kuweka mbele usawa wa kijinsia, elimu bora na uwezeshaji wa vijana, Tanzania itajenga jamii iliyo thabiti, yenye usawa na maendeleo shirikishi.

Katika utekelezaji wa dira, kila Mtanzania anawabijika kufanya kazi kwa bidii, ubunifu na kutimiza wajibu wa kiraia kama kulipa kodi, kulinda mali za umma na kushiriki kwenye uamuzi wa kijamii.

Wananchi wanapaswa kuwa walinzi wa amani, wawe mfano wa uadilifu na waendeleze mshikamano wa kitaifa.

Vilevile, ni muhimu kuendeleza uzalendo kwa kufanya kazi kwa malengo na kujituma katika sekta mbalimbali kama kilimo, biashara, elimu, teknolojia na huduma.

Mwaka 1967 Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere alizungumzia dhana ya kujitegemea kupitia falsafa yake ya Ujamaa na Kujitegemea katika hotuba yake ya 'Elimu ya Kujitegemea' (1967) na Azimio la Arusha.

Anaelezea dhana hiyo kwa upana na kusisitiza falsafa yake inalenga kujenga taifa lenye uwezo wa kujitegemea kiuchumi na kijamii, lenye uhuru na usawa, lililo tayari kuondokana na urithi wa ukoloni.

Nyerere anatetea mfumo wa elimu ambao uliendana na mahitaji halisi ya jamii, kutoa mafunzo ya kazi na kuwaandaa vijana kuendeleza na kutumikia nchi yao, mambo ambayo katika Dira ya 2050 yamebainishwa bayana kama moja ya msingi katika kuitekeleza dira.

Ndiyo maana ili dira ifanikiwe, Watanzania wanapaswa kujenga tabia ya kujitegemea kiuchumi na kijamii, kutegemea ujuzi na ubunifu wao badala ya kutegemea misaada kutoka nje.

Hii ndiyo roho ya maendeleo jumuishi na endelevu ambayo Dira ya 2050 inasisitiza.

Kwa upande mwingine, serikali ina jukumu kubwa kuratibu, kusimamia na kuweka mazingira bora ya utekelezaji wa dira.

Kwanza, inapaswa kuhakikisha sera, mipango na bajeti za kitaifa zinakwenda sambamba na malengo ya dira.

Serikali lazima iendelee kuboresha miundombinu ya kiuchumi kama barabara, reli, bandari, huduma za umeme na mawasiliano ili kuwezesha ukuaji wa sekta za uzalishaji, kuondoa umasikini na kuboresha maisha ya wananchi kwa kuongeza fursa za ajira.

Mambo hayo yamebainishwa katika vichocheo vya kufikia malengo ya dira, yakiwemo mageuzi makubwa yanayoendelea kufanyika nchini kupitia sekta ya ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji.

Aidha, kupitia sekta ya uzalishaji kwa kuhakikisha gharama za uzalishaji zinapungua na kuimarisha utendaji kazi.

Mchumi mashuhuri, Profesa Samwel Wangwe anasema Tanzania haiwezi kufikia uchumi jumuishi bila mageuzi makubwa ya kimuundo katika sekta muhimu kama kilimo, viwanda na usafirishaji.

Profesa Wangwe anasema, "Ili kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, tunapaswa kuimarisha sekta ya usafirishaji na kuiweka Tanzania katika nafasi ya kuwa kitovu cha nchi zisizo na bandari.

"Tunapaswa kuzipa kipaumbele sekta zinazounganisha viwanda, kuunda ajira na kutoa fursa za mapato ya muda mrefu".

Pia, anasisitiza umuhimu wa utawala bora na uwajibikaji katika ngazi zote za serikali.

Profesa Wangwe anasema maendeleo jumuishi hayawezi kupatikana kama serikali za mitaa hazitaelewa wajibu zilionao




katika kupambana na rushwa na kuboresha huduma kwa wananchi.

Hata hivyo, katika kutekeleza dira hiyo, sekta binafsi na asasi za kiraia zina mchango kama washirika wa maendeleo.

Ili dira ifanikiwe, serikali inapaswa kuendelea kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji, huku sekta binafsi ikiwekeza katika viwanda, kilimo cha kisasa, teknolojia na huduma za kijamii.

Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) na Wizara ya Uwekezaji zina jukumu la kuvutia wawekezaji wa ndani na wa nje, kuhakikisha ushindani wenye tija na kukuza ajira kwa vijana.

Asasi za kiraia na wadau wa maendeleo nao wanapaswa kushiriki kutoa elimu ya uraia, ufuatiliaji wa utekelezaji wa dira na kutoa sauti kwa makundi maalumu kama wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, kuhakikisha hakuna anayeachwa nyuma.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPPC), David Kafulila anasisitiza kuwa sekta binafsi ndiyo injini ya uchumi wa taifa.

Anasema biashara nyingi ndogo na za kati zikiwa zinamilikiwa na wanawake na vijana, zinapaswa kupewa nafasi kubwa zaidi.

"SMEs (Biashara Ndogo na za Kati) ni uti wa mgongo wa uchumi wetu. Ili kufikia uchumi wa Dola trilioni moja ifikapo mwaka 2050, tunapaswa kujenga mazingira rafiki kwa biashara zinazoongozwa na wananchi kukua na kustawi," anasema.

Kafulila anabainisha mafanikio makubwa katika sekta mbalimbali, zikiwemo za wachimbaji wadogo kuongeza mchango katika mapato ya madini kutoka asilimia 20 mwaka 2021 hadi asilimia 40 mwaka 2025.

Kwa mujibu wa Kafulila, eneo la kilimo cha umwagiliaji limeongezeka kutoka hekta 500,000 mwaka 2021 hadi hekta 980,000 mwaka 2025, huku biashara za kimataifa zikiongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 17 hadi 34.

Hata hivyo, Kafulila anaweka wazi kuwa, Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) si ubinafsishaji kama wengi wanavyodhani.

Anasema, "PPP si ubinafsishaji; serikali inabaki mmiliki wa mali, huku sekta binafsi ikileta mtaji, utaalamu na teknolojia..."

Anaongeza: "Mfano mzuri ni Bandari ya Dar es Salaam ambako mfumo huu unatekelezwa kwa mafanikio na unatarajiwa kupanuliwa hadi Bagamoyo na Tanga".

Dira hiyo pia ina nguzo tatu kuu ambazo ni pamoja na uwezo wa watu na maendeleo ya jamii.

Katika hili, watu ndio moyo wa maendeleo. Dira ya 2050 inatambua kuwa maendeleo ya nchi hayawezi kufikiwa bila wananchi wenye elimu, afya njema na ustawi wa jamii.

Kuhusu elimu, dira inasisitiza elimu bora, jumuishi na yenye stadi za maisha ili kuhakikisha kila mtoto wa Kitanzania anapata elimu itakayomuwezesha kushindana katika soko la ajira la kimataifa.

Katika sekta ya afya, serikali inakusudia kutoa huduma bora za afya kwa wote, kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa na miundombinu pamoja na kuhakikisha kila mwananchi anapata bima ya afya, mpango wa afya kwa wote.

Aidha, sera ya kilimo itabadilishwa ili kusaidia wakulima kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kama ukame na mafuriko.

Hii itasaidia kujenga uchumi unaohimili misukosuko ya mazingira na kuhakikisha usalama wa chakula kwa taifa.

Maendeleo endelevu hayawezi kuwepo bila amani na utawala bora. Nguzo hii katika dira inalenga kuimarisha mifumo ya haki, uwajibikaji wa viongozi na ushiriki wa wananchi katika maamuzi.

Ushiriki wa pamoja, nidhamu ya kazi na uadilifu ndivyo vitakavyoifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati wa juu ifikapo mwaka 2050.

Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ni mwaliko wa kizazi cha sasa kuwekeza kwa ajili ya vizazi vijavyo. Ni dira inayojenga matumaini ya taifa lenye uchumi wa kisasa, watu wenye afya na elimu bora, mazingira salama na utawala unaojali watu wake.

Kila Mtanzania anapaswa kushiriki kufanya dira hiyo kuwa halisi kwa kufanya kazi kwa uadilifu, kutumia fursa zilizopo na kulinda amani ya nchi.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA

# Awamu ya Sita ilivyochangia mageuzi katika sekta ya Ushirika

**1. MAFANIKIO YA SEKTA YA USHIRIKA KATIKA SERIKALI YA AWAMU YA SITA (2021/2022 - 2024/2025)**

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania ni Idara ya Serikali inayojitegemea iliyo chini ya Wizara ya Kilimo iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 ili kutekeleza majukumu ya Udhibiti na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika pamoja na Uhamasishaji wa Maendeleo ya sekta ya Ushirika nchini.

**2. MAFANIKIO YA SEKTA YA USHIRIKA**

Katika kipindi cha miaka minne (2021/22 - 2024/25) chini ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Sekta ya Ushirika imepata mafanikio yafuatayo:

**2.1. Kuimarika kwa utendaji wa vyama vya Ushirika**

Kutokana na kuimarishwa kwa usimamizi, Vyama vya Ushirika vimeendelea kuimarika katika utekelezaji wa shughuli zake kama ilivyobainishwa na Shirika la Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika (COASCO).

Vyama vya Ushirika vilivyopata Hati safi vimeongezeka kutoka vyama 339 mwaka 2021/22 hadi kufikia vyama 631 Mwaka 2023/24. Aidha, Vyama vilivyopata Hati isiyoridhisha na maoni vimepungua kutoka Vyama 1,198 mwaka 2021/22 hadi vyama 263 mwaka 2023/24 na Hati mbaya zimepungua kutoka vyama 2,075 mwaka 2021/22 hadi 995 mwaka 2023/2024. Hali hii inaashiria kuwa utendaji wa vyama vya ushirika umeimarika.

**2.2. Kuimarika kwa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo**

Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) vimeendelea kuwahudumia wanachama wake kwa kuendelea kutoa huduma mbalimbali kama vile kutunza mali zinazomilikiwa na Vyama husika, kupokea Akiba na Amana za wanachama pamoja na kutoa mikopo yenye masharti nafuu. Hadi kufikia mwaka 2024/2025, Jumla ya Mali zilizokuwa zikimilikiwa na SACCOS zilikuwa zimeongezeka kutoka Shilingi Bilioni 836.74 kwa Mwaka 2021/2022 na kufikia Jumla ya Mali zenye thamani Shilingi Trilioni 1.46 kwa Mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 74.48, Akiba na Amana za wanachama zilikuwa zimeongezeka kutoka Shilingi Bilioni 576.01 mwaka 2021/2022 na kufikia Shilingi Trilioni 1.056 mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia 83.33. Aidha, Mikopo iliyotolewa kwa wanachama wa SACCOS ilikuwa imeongezeka kutoka Shilingi Bilioni 798.0 mwaka 2021 na kufikia Shilingi Trilioni 1.2 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 52.75.

**2.3. Kuimarika kwa Matumizi ya Mifumo rasmi ya Masoko ya Mazao ya Wakulima**

Wakulima wameendelea kukusanya na kuuza mazao yao kupitia mifumo rasmi ya masoko inayotumika katika Vyama vya Ushirika. Kuongezeka kwa mauzo kupitia Mifumo rasmi ya Ushirika kumesababisha mazao yanayouzwa kuongezeka na bei za mazao kupanda. Hadi kufikia Februari, 2025, jumla ya tani 2,225,397.56 zenye thamani ya Shilingi Trilioni 4.2 zilikusanywa na kuuzwa kupitia mfumo rasmi wa Ushirika ukilinganisha na Tani 591,268.122 zilizouzwa kwa thamani ya Shilingi Trilioni 1.1 mwaka 2021/2022.

**2.4. Kuongezeka kwa Upatikanaji na Usambazaji wa pembejeo za kilimo kupitia Vyama vya Ushirika**

Thamani ya pembejeo za kilimo zilizonunuliwa na kusambazwa kupitia Vyama vya Ushirika imeongezeka kufikia Shilingi 685,900,000,495 msimu wa 2024/25 ikilinganishwa na pembejeo zenye thamani ya Shilingi 194,167,853,651.40 kwa msimu 2021/2022. Pembejeo zilizonunuliwa na kusambazwa kwa wakulima ni mbolea, viuatilifu (dawa), vifungashio, mbegu na miche kwa ajili ya mazao ya kahawa, pamba, korosho, tumbaku, ufuta, alizeti, mahindi na mpunga.

**2.5. Ongezeko la viwanda vinavyomilikiwa na Vyama vya Ushirika**

Hadi kufikia mwaka 2024/25, jumla ya viwanda vinamilikiwa na Vyama vya Ushirika vimefikia 331 ukilinganisha na viwanda 267 mwaka 2021/2022. Shughuli zinazofanywa na viwanda hivi ni uchambuaji wa pamba, ukoboaji wa mpunga, kahawa na mahindi, usindikaji wa maziwa, ukamuaji wa mafuta ya pamba, alizeti, karanga na ufuta, na ubanguaji wa korosho.

**2.6. Kuongezeka kwa ajira katika Vyama vya Ushirika**

Kuimarika kwa Vyama vya Ushirika kumefanikisha kuongezeka kwa wananchi walioajiriwa katika vyama hivyo kufikia 155,106 mwaka 2024/2025 ikilinganishwa na wananchi 100,100 waliopata ajira katika vyama mwaka 2020/21, ikiwa ni ongezeko la asilimia 55.1.

**2.7. Kuongezeka kwa matumizi ya TEHAMA katika uendeshaji wa shughuli za Ushirika na matumizi ya mizani ya kidijitali**

2.7.1. Kuanzisha Mfumo wa Kidijitali wa Usimamizi wa Vyama




*Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan akipokea Tuzo kwa kutambua mchango wake muhimu katika Maendeleo ya Ushirika nchini. Tuzo hiyo ilikabidhiwa na Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe kwenye uzinduzi wa Benki ya Ushirika*

Katika kuimarisha usimamizi wa Vyama vya Ushirika kwa njia ya TEHAMA, Tume imeanzisha Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU) ambao umeunganishwa na Mifumo ya Taasisi 11 ambayo ni Mfumo Mkuu Unganishi wa Serikali (GovESB), Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimali (ERMS), Mfumo wa Ukusanyaji wa Malipo ya Serikali Kielektroniki (GePG), Mfumo wa Wizara ya Kilimo (e-Kilimo), Mfumo wa Mizani ya kidigitali (Mkulima Hub), Mfumo wa Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF), Mfumo wa Bodi ya Sukari (CANGROWERS-MIS), Mfumo wa ELCT ND SACCOS, Mfumo wa SCULT (SOMA), Mfumo wa Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEMIS), Mfumo wa Kutuma Jumbe wa eGA (mGov), Mfumo wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA). Aidha, mpaka sasa Vyama 6,855 vimesajiliwa kwenye MUVU ambapo Vyama vya msingi ni 6,292, Vyama vya upili ni 76, vyama vya awali ni 486 na shirikisho ni kimoja (1).

2.7.2. Kuimarika kwa matumizi ya Mizani za Kidijitali

Katika kuimarisha matumizi ya mizani za kidijitali katika ununuzi wa mazao ya wakulima msimu wa 2024/2025, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2025 jumla ya Mizani za Kidijitali 4,634 kati ya 6,184 iliyokuwa imepangwa kununuliwa ikiwa na thamani ya Shilingi Bilioni 15.16, ilinunuliwa na kusambazwa kwenye Vyama vya Ushirika Vya Ushirika vya Msingi (AMCOS) 1,661 ikilinganishwa na msimu wa 2023/2024 ambapo Vyama vya Ushirika vilikuwa na mizani za kidijitali 1,178. Mizani hiyo inatumika na AMCOS zinazojishughulisha na mazao ya kahawa, korosho, ufuta, soya, mbaazi, kakao na tumbaku katika Mikoa ya Kagera, Lindi, Mbeya, Tabora, Mtwara, Ruvuma na Pwani.

**2.8. Kuimarisha Uwekezaji wa mali za Ushirika katika uzalishaji**

Katika mwaka 2024/25, Tume imeendelea kusimamia Vyama vya Ushirika kutambua na kuthaminisha mali za kudumu za Vyama ambazo zilikuwa zimechukuliwa na kutumika nje ya utaratibu. Hadi kufikia Februari 2025, jumla ya Vyama vya Ushirika 673 vimetambua, kuthaminisha na kuingiza mali 4,348 kwenye Mfumo wa MUVU, zenye thamani ya soko ya Shilingi 1,318,807,288,055. Aidha, kwa sasa zoezi la utambuzi na uthaminishaji wa mali za kudumu za Vyama vya Ushirika linaendelea kuratibiwa kupitia Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania (TFC) na kutekelezwa na Kampuni ya World Map International.

# PONGEZI



**Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mwenyekiti wa Kamisheni, Menejimenti na Watumishi wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika tunakupongeza kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
***"Kazi na Utu, Tunasonga Mbele"***

**2.9. Kuanzishwa kwa Benki ya Ushirika**

Benki ya Ushirika Tanzania ilianzishwa kwa kuunganisha iliyokuwa Benki ya Ushirika Mkoa wa Kilimanjaro Ltd (KCBL) pamoja na Benki ya Wananchi Tandahimba Ltd (TACOBA). Benki hii ilisajiliwa mnamo 26 Mei, 2024 na Mrajis wa Vyama vya Ushirika na kupewa leseni ya uendeshaji wa biashara za mabenki kutoka kwa Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania mnamo 4 Oktoba 2024. Benki ya Ushirika ilizinduliwa na Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan, Aprili 28, 2025 na imeanza na matawi manne (4) (tawi la Dodoma, Kilimanjaro, Tabora na Tandahimba) na inamilikiwa na Vyama vya Ushirika kwa asilimia 51 kama wawekezaji wakuu. Uwekezaji wa hisa katika benki umeongezeka kutoka bilioni 15.7 2022/2023 hadi kufikia bilioni 39.4 mwaka 2024/2025. Kuanzishwa kwa Benki ya Taifa ya Ushirika kutaviwezesha Vyama vya Ushirika kufanya biashara, kupata mikopo yenye riba nafuu na kuviwezesha kujiendesha kibiashara na kuwalinda wanaushirika wakiwemo wakulima, kutokunyonywa na taasisi za fedha zinazotoa mikopo yenye riba kubwa.

**2.10. Tume imeboresha Sheria ya Ushirika**

Tume imeboresha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na 6 ya Mwaka 2013 kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Na. 1 ya Mwaka 2025. Kwa kuzingatia marekebisho tajwa, Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya Mwaka 2013 inatarajiwa kuimarisha usimamizi na udhibiti wa vyama vya ushirika, pamoja na kuvisaidia vyama kujiendesha kibiashara na kukidhi matakwa ya uanzishwaji wa Benki ya Ushirika.

**2.11. Kuimarika kwa Taswira Chanya ya Ushirika**

Kutokana na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika utekelezaji wa vipaumbele vya Sekta ya Ushirika, taswira ya Ushirika imeendelea kuimarika. Mafanikio ya Ushirika yaliyopatikana na kutangazwa kwa umma ni pamoja na kuanzishwa kwa Benki ya Ushirika, kuanzishwa kwa Mfumo wa Kidijitali wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU), Matumizi ya Mizani za Kidijitali katika mauzo ya mazao ya wakulima, Uwazi katika Minada ya mazao ya wakulima, Ongezeko la bei ya mazao yaliyouzwa kupitia Ushirika; Tumbaku, Korosho, Pamba, Kahawa, Ufuta, Kakao, Mkonge, Chai, Mbaazi, Soya, Dengu na Miwa. Wananchi wengi wameendelea kujiunga kwenye Vyama vya Ushirika ili kupata nguvu ya pamoja ya soko la mazao yao na kuongeza kuimarisha uchumi wao na Taifa kwa ujumla.

MAMLAKA YA UWEKEZAJI NA MAENEO MAALUM YA KIUCHUMI TANZANIA (TISEZA)



# SALAMU KUTOKA MAMLAKA YA UWEKEZAJI NA MAENEO MAALUM YA KIUCHUMI (TISEZA)

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Mkurugenzi Mkuu, Menejimenti, pamoja na watumishi wote wa Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi Tanzania (TISEZA), tunapenda kutoa salamu za pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Awamu ya Sita pamoja na Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

TISEZA tunatambua kwa heshima kubwa dhamira, ujasiri na uongozi bora wa Mheshimiwa Rais katika kuendeleza dira ya maendeleo ya taifa letu kupitia sera imara za kiuchumi, maboresho ya mazingira ya biashara na uwekezaji, pamoja na kuimarisha ustawi wa wananchi. Kuchaguliwa kwako ni uthibitisho wa imani kubwa ya Watanzania katika maono yako ya kuijenga Tanzania yenye uchumi shindani, jumuishi na endelevu.

Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi tunakiri na kupongeza juhudi zako katika kukuza sekta ya uwekezaji, kuimarisha miundombinu ya kiuchumi, na kuhimiza ushirikiano wa sekta binafsi na umma katika kuharakisha maendeleo. Uongozi wako umekuwa chachu ya matumaini, uthubutu na mabadiliko chanya katika nyanja mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

Kwa heshima, TISEZA tunaahidi kuendelea kuwa mshirika madhubuti wa Serikali yako Tukufu katika utekelezaji wa dira ya maendeleo ya taifa, kupitia uboreshaji wa maeneo maalum ya kiuchumi na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje. Tunakusudia kuunga mkono jitihada zako kwa vitendo katika kujenga Tanzania yenye uchumi wa viwanda, fursa sawa, na ustawi wa wote.

Tunakuombea afya njema, hekima, na uongozi wenye baraka ili uendelee kuiongoza nchi yetu kwa amani, umoja, na mafanikio makubwa zaidi.

Imetolewa na:
Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo
Maalum ya Kiuchumi Tanzania (TISEZA)
Makao Makuu
S. L. P. 938
Jengo la Golden Jubilee,
Ghorofa ya Kwanza, Mtaa wa Ohio,
Dar es Salaam.
Barua pepe: info@tiseza.go.tz
Simu: +255 734 989 470
Tovuti: www.tiseza.go.tz

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni



# SALAMU ZA PONGEZI

Mkurugenzi, Menejimenti na Watumishi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni tunaungana na Watanzania wote kukupongeza **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

# Uapisho wa Rais na Makamu wa Rais katika picha

















# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA TAIFA YA TAKWIMU

# SALAMU ZA PONGEZI





Menejimenti na Watumishi wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu wanaungana na Watanzania wote kumpongeza **Mhe. Dkt.Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamu wake **Mhe. Dkt. Emmanuel John Nchimbi** kwa kuchaguliwa kwa kishindo kwenye Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2025 ili kuendelea kuiongoza nchi yetu.

**NBS itaendelea kushirikiana na Wizara, Taasisi za Serikali na wadau wengine wa maendeleo** kwa kufanya Sensa na Tafiti mbalimbali zaKiuchumi, Kijamii na za Mazingira ili kupata Takwimu na viashiria muhimu kwa ajili ya kupanga, kupima, kufuatilia na kufanya tathmini ya Programu za Maendeleo nchini ikiwemo Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2050, Dira ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2050, Dira ya Afrika ya Mwaka 2063 na Maendeleo Endelevu ya Dunia ya Mwaka 2030.

***#KAZI NA UTU. TUNASONGA MBELE***
***TAKWIMU KWA MIPANGO JUMUISHI NA MAENDELEO ENDELEVU***

**Imetolewa na Mtakwimu Mkuu wa Serikali**
**Ofisi ya Taifa ya Takwimu**

nbs.tanzania NationalBureauofStatistcs NBSTanzania



Tunakuahidi Ushirikiano wakati wote wa Uongozi wako

Salamu za

# PONGEZI

kwa Bunge la 13



Tunawapongeza kwa dhati wabunge wote waliochaguliwa na kuteuliwa kuingia katika Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ushindi wenu ni matokeo ya imani kubwa ya wananchi waliowaamini kuwa mna uwezo wa kuwasemea, kuwatetea na kusukuma mbele masuala ya maendeleo ya taifa letu.Huu ni wakati wa kutimiza ahadi, kudumisha umoja na kuonesha uzalendo katika utumishi wa umma.

Wananchi wanawategemea kama sauti yao ndani ya Bunge. Wanawategemea muwe sauti ya ukweli, uwajibikaji na ubunifu. Wana imani kuwa mtatumia fursa hii kujadili hoja zenye kujenga, kupitisha sheria zenye manufaa kwa wote, na kusimamia utekelezaji wa sera za maendeleo kwa uadilifu.

Tunawakumbusha kuwa Bunge ni mhimili muhimu wa demokrasia hivyo, mshikamano wenu na moyo wa ushirikiano na Serikali utasaidia kuendeleza Tanzania yenye amani, umoja na ustawi. Kwa niaba ya Watanzania wote, tunawatakia kila la heri katika majukumu yenu mapya na mtangulize maslahi ya taifa. Hongera sana, Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la 13.



# Salamu za Pongezi

Kwa heshima na taadhima, kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Watumishi wote wa Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN), napenda kumpongeza kwa dhati Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ushindi wake mkubwa baada ya kuchaguliwa tena kuendelea kuongoza taifa letu katika kipindi cha pili.

Mhe. Rais, katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wako thabiti, Serikali ya Awamu ya Sita imekuwa bega kwa bega na TSN katika kila hatua ya kujenga taasisi imara, ya kisasa na yenye mchango mkubwa katika maendeleo ya taifa.

Uongozi wako wenye maono umewezesha kampuni yetu kupiga hatua kubwa katika maeneo ya ubunifu, uboreshaji wa miundombinu, na kuimarika kwa huduma za habari na mawasiliano kwa wananchi.

Kupitia uongozi wako, Serikali imewezesha utekelezaji wa miradi mikubwa kama ujenzi wa kiwanda cha uchapaji wa kibiashara cha TSN, ajira mpya kwa watumishi wenye weledi, na uwekezaji katika teknolojia ya kisasa ya uchapaji na usambazaji wa habari.

Hatua hizi zimeiwezesha TSN kuwa chombo cha habari kinachotambulika si tu nchini, bali pia katika ukanda wa Afrika Mashariki na kimataifa.

Tunashukuru kwa imani uliyoonesha kwa TSN na kwa dhamira yako ya dhati ya kuiimarisha tasnia ya habari nchini. Kwa niaba ya timu yote ya TSN, nakuhakikishia kuwa katika kipindi hiki kipya cha uongozi wako, tutaendelea kufanya kazi kwa ufanisi, weledi na ubunifu mkubwa zaidi, tukihakikisha tunakuwa daraja imara kati ya serikali na wananchi katika kuelimisha, kuhabarisha na kuhamasisha maendeleo ya taifa.

Hongera sana Mhe. Rais kwa ushindi wako. Mungu aendelee kukuongoza katika kulijenga taifa letu.

Imetolewa na:
Asha Dachi
Mkurugenzi Mtendaji, Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN).

# Ijue Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) inavyopaa katika soko la habari



***- Na Mwandishi Maalumu -***

Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) ilianzishwa mwaka 1930 wakati wa utawala wa kikoloni kwa lengo la kuchapisha na kusambaza taarifa rasmi za serikali kwa umma.

Kampuni hii kongwe imekuwa chombo kikuu cha serikali katika kutoa habari kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza kupitia magazeti yake ya Daily News, Sunday News, Daily News – EAC Edition, HabariLEO, HabariLEO Afrika Mashariki na SpotiLeo.

Kwa sasa TSN imepanua huduma zake hadi uchapaji wa kibiashara, matangazo na usambazaji wa habari kwa njia za kidijitali kupitia tovuti na mitandao ya kijamii kama Facebook, X, Instagram na YouTube.

TSN imeendelea kung'ara katika soko la habari ndani na nje ya Tanzania kutokana na mikakati madhubuti chini ya Bodi ya Wakurugenzi inayoongozwa na IGP mstaafu, Said Mwema na Menejimenti chini ya Mkurugenzi Mtendaji, Asha Dachi.

Mafanikio haya yametokana na juhudi za Serikali kuimarisha kampuni kupitia miradi mbalimbali kama Uchapaji Kibiashara, Utengenezaji wa Vipindi Maalumu, Matangazo ya magazetini na mtandaoni, Ushauri wa Kitaalamu wa Habari, Majukwaa ya Biashara, Maktaba ya Kidigitali na Ushirikiano na wadau.

Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan imewezesha utekelezaji wa mradi mkubwa wa ujenzi wa kiwanda cha uchapaji wa kibiashara (Commercial Printing), kinachotarajiwa kuwa cha kisasa zaidi barani Afrika.



**Ms Asha Dachi**
*Mkurugenzi Mtendaji - TSN*

Mradi huu utakapokamilika utarahisisha uchapaji wa magazeti, vitabu, majarida, vipeperushi, mabango na nyaraka za serikali na binafsi kwa ubora wa juu, hivyo kuifanya TSN kuwa kitovu cha uchapaji wa kitaifa na kimataifa.

Mbali na uchapaji, TSN inatoa huduma za ushauri wa kitaalamu kwa taasisi za umma na binafsi kuhusu mawasiliano na uhusiano kwa umma.

Huduma hii inajumuisha utengenezaji wa vipindi vya elimu kwa umma, makala, sera na mikakati ya mawasiliano, ili kusaidia taasisi kuwa na mifumo rasmi na kupunguza changamoto za mawasiliano kazini.

Aidha, kupitia Majukwaa ya Biashara, TSN imekuwa ikikutanisha wadau wa sekta mbalimbali kujadili fursa za uwekezaji na biashara, yakihusisha washiriki 1,000 hadi 1,500 kutoka sekta binafsi, taasisi za umma na watunga sera.

Vilevile, Maktaba ya Kidijitali ya TSN imehifadhi picha na kumbukumbu muhimu za kihistoria, ikiwemo za viongozi, harakati za ukombozi na matukio muhimu kabla na baada ya Uhuru.

Kwa ushirikiano wa Serikali, TSN imeongeza idadi ya watumishi wenye taaluma mbalimbali, hatua iliyoimarisha utendaji kazi na upashanaji wa habari kati ya serikali na wananchi. Hivi sasa kampuni ina waandishi katika kila mkoa, jambo linalorahisisha upatikanaji wa taarifa kutoka maeneo yote ya nchi.

TSN imeendelea kutumia vyombo vyake kuelimisha na kushirikisha wananchi katika miradi ya maendeleo, ikiwemo programu maalumu ya kurekodi historia ya viongozi wastaafu kwa kwa mahojiano maalumu.

Viongozi kumi (10) wamehojiwa, akiwemo Rais mstaafu wa Zanzibar, Amani Karume, Makamu wa Rais mstaafu, Dk. Mohammed Ghalib Bilal, Waziri Mkuu mstaafu, Cleopa Msuya (marehemu), Balozi Seif Ali Iddi, Spika mstaafu, Anne Makinda, Getrude Mongella na Pius Msekwa. Taarifa hizi zimehifadhiwa katika kanzidata ya TSN kama kumbukumbu muhimu za taifa.

Aidha, TSN kupitia HabariLEO na Daily News imechapisha mfululizo wa makala kuhusu maboresho ya mfumo wa kodi chini ya Tume ya Rais inayoongozwa na Ombeni Sefue, ikiwa ni sehemu ya juhudi za Rais Samia za kuimarisha mazingira rafiki ya kodi kwa wafanyabiashara. Kupitia makala hizo, wananchi walitoa maoni yao kwa Serikali.

Aidha, kupitia makala maalumu, TSN inaendelea kutangaza vivutio vya utalii na fursa mbalimbali za kiuchumi nchini, ikiunga mkono juhudi za Serikali kukuza utalii wa ndani.

Magazeti ya TSN yamekuwa chombo muhimu katika kutangaza miradi mikubwa ya kimkakati ya Serikali ya Awamu ya Sita na kueleza mafanikio ya utekelezaji wa Dira ya Maendeleo 2025 pamoja na maandalizi ya Dira 2050.

Kampuni pia ilikuwa mstari wa mbele katika kuelimisha umma kuhusu uchaguzi, uraia na umuhimu wa ushiriki katika kupiga kura, jambo lililochangia hamasa.

Baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 29, 2025, TSN imeendelea kutumia vyombo vyake kuimarisha umoja wa kitaifa kwa kuchapisha habari zinazohimiza amani, maridhiano na ushirikiano wa wananchi katika kujenga taifa lenye maendeleo endelevu chini ya uongozi thabiti wa Rais Dk Samia Suluhu Hassan.

TANZANIA STANDARD NEWSPAPER

# KATALOGI YA BIASHARA

"Kampuni ya Magazeti ya Serikali"

## Bidhaa na Huduma Zetu


- **Magazeti** na Majarida
- **Uchapishaji** wa Kibiashara
- **Epaper Gazeti** la Mtandaoni
- **Ushauri wa Vyombo** vya Habari
- **Matangazo**
- **Jukwaa la** Biashara
- **Huduma Maalum** za Vyombo vya Habari
- **Maktaba ya Kidigitali** na Upigaji Picha wa Kibiashara

## KWA NINI UTUCHAGUE SISI?

1. Chombo cha habari cha serikali.
2. Uzoefu wa miaka 90.
3. Huduma zisizo na usumbufu na uwasilishaji kwa wakati.

Mkurugenzi Mtendaji: Asha Dachi – 0786 46 71 33
Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara: Soter Salema – 0765 288 798
Meneja wa Mauzo na Usambazaji: Jonathan Manhe – 0653 912 475
Meneja wa Masoko na Utangazaji wa Bidhaa – Felix Mushi: 0754 492 310
Meneja wa Kitengo cha Uchapaji – Selemani Mwaitenga: 0745 599 029
Meneja wa Lugha za Kigeni: Christopher Majaliwa – 0714 071 525
Mkuu wa Kitengo cha Matangazo: John Koyi – 0713 598 567
Kaimu Msanifu Mkuu: Stella Nyeminohi – 0713 525 127
Msanifu Mwandamizi: Kiteja N. Mayunga – 0655 111 727

**Sisi ni Magwiji wa Uchapishaji.**




# Wadhamini